

Wasafiri wanahitaji kutambua aina ya kipimo, chanzo cha kipimo na matakwa ya nyaraka za matokeo yanayohitajika na eneo wanaloenda. Wasiliana na shirika lako la ndege au wakala wa usafiri kwa maswali kuhusu matakwa haya.

Watu binafsi wanaopimwa kwenye maeneo ya kupimia ya jamii, kwa madhumuni ya safari, wanapaswa kuwafahamisha waratibu wa eneo la kupimia wanapojisajili. Maeneo ya kupimia yanaweza kupatikana kwenye: [Maeneo ya Kupimia: Mahali pa kupata Vipimo vya COVID-19 huku North Dakota \(nd.gov\)](#)

Kupima:

- Aina ya vipimo vilivyopo:
 - RT-PCR (aina ya NAAT)
 - Inakusanywa nyuma ya koo (Oropharyngeal/OP) au nyuma ya pua (Nasopharyngeal/NP)
 - **Matokeo ya PCR yanapaswa kutarajiwa TU saa 48-72 baada ya kipimo chako kuwasili kwenye maabara.**
 - Antijeni ya haraka (**SI** kipimo cha PCR wala NAAT)
 - Inakusanywa mbele ya pua
 - Ripoti za matokeo zinapatikana ndani ya dakika 60-90
- Kabla hujapimwa, kamilisha usajili wa **Wakati Mmoja** kwenye [testreg.nd.gov](#)
 - Jina lililosajiliwa linapaswa kulingana na waraka utakaotumika kwa safari kama pasipoti yako.
 - Lazima ukubali kupokea matokeo kupitia SMS au barua pepe ili utumiwe arifa ya mtandaoni ya matokeo yako.

Jinsi ya kuyafikia MATOKEO yangu:

Maabara ya jimbo **hayachakati** vipimo siku za Jumapili. Hata hivyo, vipimo vilivyofanywa wikendi bado matokeo yavyo yapatikana ndani ya saa 48-72 kutoka wakati wa kuwasili kwenye maabara.

- **Kituo cha Raia:** Ufikiaji huru wa matokeo ya vipimo na ripoti za matokeo ya PDF zinazoweza kuchapishwa.
 - Fungua akaunti ya NDLogin wakati wa usajili au ukitumia kiungo kilicho kwenye arifa ya mtandaoni
 - Baada ya kupata matokeo ya kipimo chako, ingia katika Kituo cha Raia kwenye [testreg.nd.gov](#) ili ufikie kipimo chako na PDF inayoweza kuchapishwa
- **Utafiti wa Mtandaoni:** Kamilisha utafiti wa mtandaoni ili utumiwe nakala ya ripoti ya PDF ya matokeo yako.
 - Maombi ya utafiti yanafuatiliwa Jumatatu-Jumamosi kuanzia saa 8:00 asubuhi hadi saa 7:00 usiku
- Nenda kwenye [Matokeo ya Vipimo | Idara ya Afya \(nd.gov\)](#) kwa maelezo ya kina kuhusu kufikia matokeo

Watu binafsi wanaohitaji usaidizi wa kufikia matokeo wanaweza:

- Kupiga **Simu ya Dharura ya Matokeo** kwa nambari 701-204-6664, Jumatatu-Jumamosi kuanzia saa 8:00 asubuhi hadi saa 7:00 usiku

Matakwa ya kawaida ya kuzingatia:

Idara ya Afya ya North Dakota haiwezi kutoa nakala ya matokeo ya kipimo kilichofanywa kwenye maabara mengine wala kipimo kilichoagizwa/kilichokusanywa na mtoa huduma wa afya wa binafsi

- Safari ya kimataifa: Thibitisha ikiwa eneo unaloenda linahitaji matokeo kulingana na saa za kuondoka au saa za kuwasili. Kwa kawaida, ni saa za kuondoka lakini si wakati wote. **Thibitisha matakwa ya saa za matokeo na shirika la ndege ili kuhakikisha kipimo chako wakati unaofaa.**
- Maelezo ya demografia ya msafiri (jina, tarehe ya kuzaliwa, n.k.) kwenye usajili wa kipimo yanapaswa kulingana na waraka uliotumika kwa ajili ya safari (yaani: pasipoti).
- Nakala za matokeo zilizotolewa na maabara ya jimbo zinajumuisha maelezo kutoka kwenye usajili wa kipimo na **haziwezi** kubadilishwa baada ya kuchakatwa.
 - **Ripoti za matokeo ya PDR zinazoweza kuchapishwa za RT-PCR** kutoka kwenye maabara ya jimbo zinajumuisha: Muhuri wa Jimbo la ND, anwani ya Maabara ya Afya ya Umma ya ND, Nambari ya Sampuli, Jina la Mgonjwa, Tarehe ya Kuzaliwa, Jinsia, Chanzo cha Sampuli, Tarehe/Saa ilipopokelewa kwenye maabara, Tarehe ya Ukusanyaji, Daktari Anayeomba, Kituo Kinachoomba, Jina la Kipimo, Matokeo, Ukalimani, Tarehe ya Kupimwa, sahihi ya idhini, tarehe ya Idhini na nambari ya Cheti cha CLIA.
 - **Ripoti za matokeo za Antijeni ya Haraka** zinajumuisha: Muhuri wa Jimbo la ND, nambari ya Kitambulisho cha Kipimo, Jina Kamili, Tarehe ya Kuzaliwa, Jina la Kituo Kinachoomba, Aina ya Kipimo Kilichofanywa, Chanzo cha Sampuli, Tarehe ya Ukusanyaji Sampuli, Matokeo na Tarehe ya Matokeo.